




# Tutaondoa ufadhili kwa mashirika ya serikali yasiyo na faida – Owalo

Naibu Mkuu wa Wafanyakazi Kuhusu Usimamizi wa Utendakazi na Utekelezaji katika Ofisi Kuu ya Rais, Eliud Owalo anasema mashirika ambayo yatachangia kwa kiasi kikubwa ajenda ya maendeleo ya kitaifa yatapokea ufadhili zaidi, ilhali yasiyo na faida yataondolewa ufadhili.

**NA DANIEL IRUKAN (PCO)**  
Naibu Mkuu wa Wafanyakazi Kuhusu Usimamizi wa Utendakazi na Utekelezaji katika Ofisi Kuu ya Rais, Bw. Eliud Owalo, ametangaza mabadiliko ya kimbakati katika ufadhili wa serikali, kuambatanisha usimamizi wa utendakazi na tathmini na msaada wa kifedha.

Wizara, Idara, na Mashirika (MDAs) zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika ajenda ya maendeleo ya taifa zitapokea ufadhili zaidi, huku taasisi zinazofanya vibaya kikazi zikiwa hatarini ya kuondolewa ufadhili, alisema. “Kusonga mbele, tutafungamanisha usimamizi wa utendakazi na tathmini ya utendakazi ili kutuza

usimamizi na kutenga pesa zaidi kwa mashirika ambayo yanaongeza thamani zaidi kwa ajenda ya maendeleo ya serikali,” akasema Owalo.

Alisisitiza umuhimu wa ubunifu na kujitegemea miongoni mwa taasisi za serikali, na kuzitaka kuendeleza vyanzo huru vya mapato badala ya kutegemea hazina ya kitaifa pekee.

“Mwelekeo tunaochukua kama serikali ni kwamba hatutaruhusu mashirika yasiyofanya vizuri daima kuendelea kunyonya hazina ya kitaifa. Mashirika haya

ENDELEA UK 2

|                            |                                                                                                             |                                                                                                                                          |                                                                                                           |                                                                                                                    |                                                                                                                                                                     |
|----------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| <div>Takwimu za Wiki</div> | <div>99,875</div> <div>Tani za mbolea ambayo KTDA inapanga kunua kwa ajili ya wakulima wadogo wa chai</div> | <div>45,000</div> <div>Kilo za mbegu iliyoidhinishwa ya alizeti ambayo Serikali ya Kaunti ya Nakuru imesambaza kwa wakulima 11,900</div> | <div>4.9B</div> <div>Gharama ya barabara ya kilomita 63 ya Kisumu-Miwani-Chemelil-Muhoroni-Kipsitet</div> | <div>5B</div> <div>Kiasi cha pesa za faida ambazo kampuni ya KenGen ilipata katika mwaka wa kifedha uliopita</div> | <div>4.2B</div> <div>Gharama ya mradi wa Shirika la Reli Kenya wa kuanzisha treni ya kuhudumu kati ya kituo cha Mombasa SGR na Central Railway Jijini Mombasa</div> |
|----------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------|------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|

## KTDA kuagiza mifuko 99m ya mbolea kwa wakuuzaji chai

**NA WANGARI MWANGI, KNA**  
Shirika la Ustawi wa Chai Kenya (KTDA) litanunua mbolea kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima wadogo wa chai katika maeneo yanayokuza chai. Shirika hilo linapanga kugiza karibu tani 99,875 za mbolea aina ya NPK kwa ajili ya matumizi ya wakulima wadogo 700,000 wa chai wakati wa msimu wa kilimo cha chai wa 2025. Katika tangazo la zabuni, shirika hilo linasema kwamba

linatafuta mtengenezaji wa kimataifa au wakala aliyeidhinishwa kusambaza mbolea ya NPK 26:5:5. Shehena ya mwaka huu itajumuisha karibu mifuko milioni 1.9 ya kilo 50 za mbolea. Ununuzi huo unazidi ununuzi wa 2024 kwa tani 2,887, kwani shirika hilo lilitanunua tani 97,000 mwaka jana kupitia zabuni ya ushindani ya kimataifa kutoka Urusi. “KTDA Management Services Limited inanuia kununua karibu tani 99,875 (mifuko

1,997,500 ya kilo 50 ya mbolea ya NPK 26:5:5 iliyochanganywa na kemikali kwa wakulima wadogo wa chai katika viwanda vyake vya chai vinavyosimamiwa kote nchini Kenya kwa mwaka wa 2025,” ikasema taarifa ya shirika hilo. “Kwa hivyo shirika hili linawaalika watengenezaji na/au mawakala walioidhinishwa kutoa zabuni ya usambazaji wa mbolea hiyo kama ilivyoainishwa katika hati ya zabuni,”

ENDELEA UK 2



# Tutaondoa ufadhili kwa mashirika ya serikali yasiyo na faida – Owalo

ENDELEA KUTOKA UK 1

yanafaa kusambaratika,” akaonya Bw. Owalo aki-hutubia viongozi wa Mamlaka ya Kitaifa ya Uvunaji na Uhifadhi wa Maji (NWHSA) wakati wa tathmini ya kandarasi ya utendakazi kwa mwaka wa kifedha wa 2023/2024.

Mwenyekiti wa Bodi ya NWHSA, CPA Symon Kimaru, aliangazia uhaba wa kifedha kama kik-wazo kikubwa, akitoa mfano wa muda mrefu wa kukamilisha miradi na uhaba wa kifedha.

“Mojawapo ya changa-moto kubwa tunayokabiliana nayo kama shirika ni kwamba miradi yetu inaendeshwa kwa muda mrefu sana, na uwezo wetu wa kifedha unabakwa kila mara. Hata hatuwezi kuzindua miradi mipya kwa sababu ya ba-jeti ndogo,” akasema.

Tathmini hiyo ita-chunguza utendakazi wa NWHSA kwa kutege-mea viashirio muhimu, ukiwemo usimamizi wa fedha, ukusanyaji fedha, utoaji wa huduma, ujenzi na usimamizi wa ma-



Naibu Mkuu wa Wafanyakazi katika Ofisi Kuu ya Rais Bw. Eliud Owalo wakati wa Thamini ya Utendakazi katika Mamlaka ya Kitaifa ya Uvunaji na Uhifadhi wa Maji (NWHSA).

PICHA: HENRY KWENYA

bwawa, hatua za kudhibiti mafuriko, na uimarishaji wa usambazaji maji.

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu, Mhandisi Julius K. Mugun, alisisitiza jukumu la NWHSA chini ya Sheria ya Maji ya 2016, kuwa kuendeleza kazi za kitaifa za maji kwa ajili ya kuhi-fadhi, kudhibiti mafuriko na unyunyizaji.

Kenya imekabiliwa na uhaba wa maji kwa muda mrefu, huku asilimia 80 ya nchi ikitajwa kuwa kame au nusu kame. Mvua ni wastani wa mil-imita 630 kwa mwaka,

kuanzia chini ya 200 mm Kaskazini mwa Kenya hadi zaidi ya 1,800 mm katika nyanda za juu za Mlima Kenya.

Upatikanaji wa maji kwa kila mtu nchini, un-aokadiriwa kuwa mita za ujazo 450 mwaka wa 2021, uko chini ya kiwango cha kimataifa cha mita za ujazo 1,000. Mpango Ka-bambe wa Maji wa Kitaifa unakadiriwa kuongezeka kwa mahitaji ya maji hadi asilimia 47 ya rasilimali zilizopo ifikapo 2030, iki-chochewa na uhaba wa miundomsingi ya maji na

sera duni za uvunaji.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa ya mwaka wa 2023 inasisitiza dharura ya kimataifa, ikifichua kuwa asilimia 26 ya watu duniani hawana maji safi ya kunywa, huku asilimia 46 wakikosa huduma za usafi zinazosimamiwa kwa usalama.

Kukabiliana na changa-moto hizi, Mpango Mkakati wa NWHSA wa 2023-2027 unalenga kui-marisha hifadhi ya kitaifa ya maji kwa mita za ujazo milioni 125 kupitia miradi muhimu.

# KTDA kuagiza mifuko 99m ya mbolea kwa wakulima wadogo wa chai kote nchini

ENDELEA KUTOKA UK 1

linaongeza tangazo hilo lililochapishwa kwenye tovuti ya shirika hilo.

Kulingana na tan-gazo hilo, zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo, huku wazabuni wakipewa fursa ya kus-huhudia zabuni hiyo ikifunguliwa. “Nyaraka za zabuni zilizokamil-ishwa zinapaswa ku-wekwa kwenye sanduku la zabuni kwenye eneo la mapokezi katika ghorofa ya chini ya Majani Plaza, Mtaa wa Koinange, Nai-robi, kabla ya saa 9:30 asubuhi Saa za Afrika Mashariki mnamo Feb-ruari 25, 2025.

“Zabuni zilizowasil-ishwa zitafunguliwa siku hiyo hiyo. Wazabuni au wawakilishi wao wal-ioteuliwa wanaweza kuchagua kuhudhu-ria kupitia kiunga cha video au wao binafsi,” linasema tangazo hilo.

KTDA imekuwa ikinunua mbolea kwa wingi kwa wakulima wadogo wa chai

wanaopeleka majani mabichi kwa viwanda vinavyosimamiwa na KTDA. Mpano huu un-ahakikisha wakulima wanapata mbolea ya ubora wa juu kwa bei nafuu na kupitia mfumo unaotegemewa wa us-ambazaji.

Baada ya mbolea hiyo kuwasilishwa nchini, KTDA huifunga kwenye mifuko ya kilo 50 na kupanga bei ya reja reja kisha kuisambaza kwa wakulima kupi-tia viwanda vyao, huku ikirudisha gharama kutoka kwa mkulima wakati wa malipo.

Mwaka jana, KTDA ilisambaza mbolea hiyo kwa gharama ya Sh2,500 kwa kila mfuko wa kilo 50, kufuatia ruzuku ya mbolea ya Sh2 bilioni iliyotolewa na Wizara ya Kilimo kwa sekta ndogo ya chai. Ruzuku hii il-iruhusu wakulima ku-pata punguzo la Sh900 kwa kila mfuko wa kilo 50 wa mbolea ulionunu-liwa kiwandani.



THE MERU NATIONAL POLYTECHNIC

P.O BOX 111- 60200 Meru - Kenya

Tel: +254 719 347 059

email: [info@merunationalpolytechnic.ac.ke](mailto:info@merunationalpolytechnic.ac.ke)

Website [www.mnp.ac.ke](http://www.mnp.ac.ke)

TENDER NOTICE - RE-ADVERTISEMENT

The Meru National Polytechnic invites tenders from qualified bidders to carry out the following projects:

| TENDER NO.              | TENDER DESCRIPTION                                                                                  | CATEGORY |
|-------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------|----------|
| MNP/CONST/001/2024-2025 | TENDER FOR CONSTRUCTION OF AN AUTO-MOTIVE GARAGE AT MERU NATIONAL POLYTECHNIC (PHASE 2)             | YOUTH    |
| MNP/CONST/002/2024-2025 | TENDER FOR CONSTRUCTION OF CLASS-ROOMS & OTHER FACILITIES AT MERU NATIONAL POLYTECHNIC GIAKI CAMPUS | YOUTH    |

Interested bidders may obtain tender documents from the procurement office, Meru National Polytechnic upon payment of a non-refundable fee of **Kshs 1,000** at the cash office during normal working days. Documents can also be downloaded from the government tenders portal [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke) or from the Polytechnic's website [www.mnp.ac.ke/tenders](http://www.mnp.ac.ke/tenders).

Bidders who download the tender documents MUST forward their particulars immediately to [po@merunationalpolytechnic.ac.ke](mailto:po@merunationalpolytechnic.ac.ke) for records so as to be used for any further tender clarification and addenda. All enquiries on this tenders should be channelled through [info@merunationalpolytechnic.ac.ke](mailto:info@merunationalpolytechnic.ac.ke) / [po@merunationalpolytechnic.ac.ke](mailto:po@merunationalpolytechnic.ac.ke).

Complete documents in a plain, sealed envelope marked tender number and description should be addressed to:

**THE CHIEF PRINCIPAL  
THE MERU NATIONAL POLYTECHNIC  
P.O BOX 111 - 60200 MERU**

And deposited in the TENDER BOX at the polytechnic reception so as to be received on or before **Wednesday 26<sup>th</sup> February 2025 at 10.00 a.m.** The documents will be opened on the same day at **10:00am** in the main reception (Meru National Polytechnic) and bidders or their representatives are welcome to witness the opening.

**PROCUREMENT OFFICER  
FOR:CHIEF PRINCIPAL**



AGRICULTURE AND FOOD AUTHORITY

JOB VACANCIES

The Agriculture and Food Authority (AFA) is a State Corporation established under section 3 of the AFA Act No.13 of 2013. The mandate of AFA is to regulate the crops sector in Kenya, to ensure compliance with the regulatory framework, standards, and codes of practice. As a regulator, it fosters a thriving competitive environment where innovation, technological progress, order and quality flourish, for sustainable economic growth.

AFA is inviting applications from qualified candidates for the following positions:

| S.No. | Position                                | Grade | No. of vacancies | Terms of Service |
|-------|-----------------------------------------|-------|------------------|------------------|
| 1.    | Director Finance                        | 2     | 1                | Contract         |
| 2.    | Director Legal Services                 | 2     | 1                | Contract         |
| 3.    | Deputy Director Corporate Communication | 3     | 1                | P&P              |

**HOW TO APPLY:**

- Applicants can find a detailed advertisement and application information on AFA Website [www.afa.go.ke](http://www.afa.go.ke)
- Applications should reach us not later than **5.00pm (East African Time) on 24<sup>th</sup> February 2025**

Successfully shortlisted candidates will be required to satisfy the requirements of Chapter Six (6) of the Constitution of Kenya on leadership and integrity by submitting clearance certificates from relevant institutions.

**Note: AFA is an equal opportunity employer, therefore people with disabilities, the marginalized and the minorities are encouraged to apply. Applicants are informed that any form of canvassing will lead to automatic disqualification.**

# Serikali yatoa hati miliki 3,000 katika eneo la Garissa Mjini na kupanua haki za kumiliki ardhi

NA ERICK KYALO, KNA

**W**aziri wa Ardhi, Ujenzi, Nyumba na Ustawi wa Miji, Alice Wahome, amesisitiza ahadi ya wizara hiyo ya kutoa kwa ufanisi huduma kwa Wakenya.

Wahome alisema kuwa serikali inashughulikia mashamba sita ya ziada ya jamii ambayo haya-jasajiliwa katika Kaunti ya Garissa ambayo serikali ya Kaunti imewasilisha kuchapishwa katika gazeti la serikali.

Aliwataka wanaonufaika watumie hati miliki zao kwa uwajibikaji na kuepuka kuuza ardhi yao kiholela. “Tangu uhuru, ni hati miliki 3,000 pekee ambazo zimetolewa kwa watu wa Garissa. Leo pekee, tunatoa nyingine 3,000 kwa wakazi wa Garissa Mjini, na hati miliki 4,500 zaidi zinazotayarishwa kwa sasa,” akasema Wahome.

“Utarishaji wa hati miliki ni muhimu kwa sababu unatoa nyaraka za kisheria za umiliki wa ardhi, kuhakikisha usalama wa umiliki, kuwezesha shughuli za ardhi, na kuwezesha upatikanaji wa mikopo. Hatimaye, unachangia maendeleo ya kiuchumi na kupunguza umaskini,” akaongeza.

Utoaji wa hati miliki katika eneo hilo utakuwa na mchango mkubwa ka-



**Rais William Ruto na maafisa wakuu wa serikali wakati wa kutoa hati miliki 3,000 kwa wakazi wa Kaunti Ndogo ya Garissa Mjini. Picha/Erick Kyalo**

tika kuboresha usalama na kukuza mshikamano kwa kuondoa mizozo ya mara kwa mara ya ardhi, ambayo imesababishwa na kukosekana kwa uhalali wa kisheria katika madai ya kumiliki ardhi.

Katibu Mkuu wa Ardhi na Mipango ya Ujenzi, Nixon Korir, alimshukuru Rais William Ruto kwa

kutanguliza umiliki wa ardhi katika Kaunti ya Garissa.

**“Tangu uhuru, ni hati miliki 3,000 pekee zimetolewa kwa wakazi wa Garissa**

“Mbali na hati miliki 3,000 zilizotolewa, leo, tuna 1,034 zaidi zinazosubiri kutiwa saini na zingine 3,543 zinazotayarishwa,” akasema Katibu Mkuu Korir.

Waziri na Katibu Mkuu walikuwa wakizungumza mjini Garissa ambapo Rais alitoa hati miliki 3,000 kwa wakazi wa se-

hemu tano katika Kaunti Ndogo ya Garissa, Kaunti ya Garissa, akithibitisha tena dhamira ya serikali ya kuboresha usalama wa umiliki wa ardhi kwa Wakenya wote.

Hati miliki hizo zili-gawiwa walengwa kutoka Manispaa ya Garissa Kitalu nambari 3, 6, 7, 8, na 9, kuashiria hatua mu-

himu katika mageuzi ya ardhi na haki za umiliki katika eneo hilo.

Rais pia alizindua Mradi wa Nyumba za bei nafuu wa Garissa, ambao unajumuisha nyumba 408.

Mradi huo unatarajiwa kuchechea uchumi wa eneo hilo kwa kuunda nafasi za ajira na kutoa nyumba nzuri na za bei nafuu kwa wakazi wa eneo hilo.

Rais alikuwa ameandamana na viongozi wakuu wa serikali, akiwemo Naibu Rais Kithure Kindiki, Waziri wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misituta, Aden Duale, Makatibu Wakuu, Nixon Korir (Ardhi na Mipango ya Ujenzi), Charles Hinga (Nyumba na Maendeleo ya Miji), Abubakar Hassan Abdi (Ukuzaji wa Uwekezaji), Chris Kiptoo (Hazina ya Kitaifa) Mohamed Daghar (Uchukuzi) na Jonathan Mueke (Ustawi wa Mifugo).

Viongozi wengine waliokuwepo ni Magavana Nathif Jama (Garissa) na Mohamud Ali (Marsabit) Seneta wa Garissa Abdul Haji, Mwakilishi wa Wanawake wa Garissa Anab Gure, Wabunge Farah Maalim (Daadab), Shurie Abdi Omar (Balambala), Salah Yakub (Fafi) na Mohamed Abdikadir (Lagdera).



KESRA Centre  
Westlands, off Waiyaki Way  
Tel : 0709 752 727 / 0715 877 539



**CORPORATE TRAINING 2025**

## FEBRUARY PROGRAMS

| PROGRAM                                                         | TARGET AUDIENCE                                                                                                                                             | DATE        | VENUE   |
|-----------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------|---------|
| Corporate Planning & Strategy Development                       | Board members, C-level executives, Organizational Top/Senior Management, Financial controllers, Strategy & Planning Section Teams.                          | 17th - 21st | Mombasa |
| Economic Diplomacy and Negotiation                              | Diplomats, International Relations professionals, Managers, Project Leads, Trade & Finance Experts.                                                         | 17th - 21st | Mombasa |
| Organizational Productivity, Performance Management & Analytics | HR Practitioners, Performance Management Champions, Finance, Strategy, Budget & Planning Staff, Data Analysts, Process Engineers, Business Policy Analysts. | 17th - 28th | Mombasa |
| Debt Management, Enforcement And Sustainability Program         | Revenue & Finance Officers, Debt Managers, Debt Agencies, SACCOs & Banks, Debt Policy and Economic staff, Credit Managers                                   | 17th - 28th | Mombasa |
| Customs Logistics and Procedures                                | Customs Agencies, Traders, Clearing Agents, Shipping & Forwarding Agents, Logisticians.                                                                     | 24th - 28th | Nairobi |
| Tax Matters and Financial Reporting                             | CFOs, Auditors, Accountants, Finance Professional, Business Owners, Tax Professionals.                                                                      | 24th - 28th | Mombasa |

## MARCH PROGRAMS

| PROGRAM                                                      | TARGET AUDIENCE                                                                                                                                                                                  | DATE        | VENUE   |
|--------------------------------------------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------|---------|
| Tax Administration                                           | Heads of Departments, Tax/Accountants/Finance Officers, Payroll Officers, Treasury/Revenue Officers, Auditors, Tax Consultants / professionals, Business owners.                                 | 17th - 21st | Mombasa |
| Tariff Classification and Customs Procedures                 | Customs/Freight brokers, Clearing Agents, Importers and Exporters, Freight and Logistics staff, Manufacturing & Processing, Freight Logistics Regulatory bodies, Oil Marketers and Transporters. | 17th - 21st | Mombasa |
| Revenue Automation, Innovation and Data Governance           | Chief Officers, Directors, Heads of departments, SROs, Revenue officers, Members of the County Assembly (MCAs).                                                                                  | 17th - 28th | Mombasa |
| Legislative, Diplomacy and Leadership Program for Assemblies | CASB Committee members, Assembly Departmental Committees, Assembly Clerks, Deputy Clerks & Heads of Directorates, PFO, PHRO, Chief Internal Auditors, Heads of Departments in the Assemblies.    | 17th - 28th | Mombasa |
| Integrated Customs Management Systems (ICMS)                 | Customs Agents, Importers/Exporters, Shippers, Finance/ Revenue Officers, Accountants, Auditors, Inspection Agencies, Trade, Aviation & Immigration staff, Tax Consultants, Bond Processors.     | 25th - 30th | Blended |

**REGISTER TODAY**



# Katibu Mkuu aonya waajiri kuhusu malipo duni kwa wafanyakazi wao

NA CATHERINE KAMAU (PCO)

**K**atibu Mkuu wa Leba Shadrack Mwadime amewaonya waa-jiri, huswa wa sekta ya maduka makubwa na sekta nyingine, dhidi ya malipo duni ya wafanya-kazi.

Alisisitiza kuwa serikali imepanga kuwachukulia hatua za kisheria wataka-oshindwa kuzingatia kan-uni za mishahara. Kauli ya Mwadime ilifuatia mku-tano na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP) Renson Igonga, ambao uli-husu utekelezaji wa sheria za kazi.

Katibu Mkuu alisisitiza umuhimu wa kulinda haki za wafanyakazi, akisema biashara zinazokiuka sheria za mishahara zi-tachukuliwa hatua. “Tu-natoa onyo kwa waajiri wasio waaminifu. Wale wanaoendelea kunyanyasa wafanyakazi kwa kulipa chini ya kima cha chini kilichowekwa wajue siku zao zimehesabiwa. Serikali imejitolea kutekeleza sheria za kazi, na wa-takaopatikana watakabili- iwa kikamilifu kisheria,” akasema Mwadime.

Kampuni na mashirika mengi kwa sasa yanata-tizika kutimiza majukumu yake ya malipo. Kulingana na Wizara ya Kazi, walio-athirika zaidi ni pamoja na kampuni za usalama, maduka makubwa, na kampuni ya biashara ya utayarishaji wa mauzo.



**Katibu Mkuu wa Leba Shadrack Mwadime na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP) Renson Igonga wakati wa mkutano wa kujadili jinsi ya kutekeleza sheria za kazi. Picha/Catherine Kamau**

“Wafanyakazi wanasta-hili fidia ya haki kwa kazi yao ngumu,” akasema Mwadime.

Kwa kuzingatia suala hili, serikali imeashiria kwamba kutaja hadharani na kuaibisha kampuni

**Wale ambao wanan-yanyasa wafanyakazi wajue siku zao zimehesabiwa – Katibu Mkuu**

hizi kutatumika kama ujumbe wenye nguvu ku-husu umuhimu wa kuzin-gatia kima cha chini cha mishahara kilichowekwa kisheria.

Uamuzi huu unasisitiza hitaji la haraka la kufuata kanuni zinazosimamia malipo ya wafanyakazi. Wizara pia imeelezea wasiwasi kuhusu kampuni katika maeneo yao ya kazi, ikionya kuwa ukaidi huo hautapita bila kuadhibiwa.

“Haikubaliki kwamba

biashara zingine zina-wanyima maafisa wetu kuchunguza ustawi wa wafanyakazi. Tutahakik-isha kwamba taasisi hizi zinawajibishwa. Waa-jiri lazima wazingatie matakwa ya kisheria au wawe tayari kushtakiwa,” akasema Katibu Mkuu.

Serikali pia imeahidi kutayarisha mwongozo wa mtumiaji ili kusaidia maafisa wake katika kus-imamia ipasavyo kesi za kisheria.

Mwadime amewataka waajiri wote wazingatie sheria na kuwaheshimu wafanyakazi wao huku akitahadharisha kuwa kutotekeleza sheria hiyo kutasababisha madhara makubwa kisheria. “Mishahara ya haki na mazingira mazuri ya kazi ni mambo yasiyoweza kujadiliwa. Ukikataa kufuata sheria, sheria itakukamata,” akasisitiza.

Katika kikao hicho, Ig-onga alisema ofisi yake itaanza kuwafungulia mashtaka wanaokiuka sheria za kazi, vikiwemo visa vya wizi wa mishahara na unyanyasaji wa aina nyingine katika se-hemu za kazi. “ODPP in-asalia na nia ya kushikilia mamlaka yake ya kikatiba chini ya Ibara ya 157(6) ya katiba ya kuanzisha kesi za jinai na kuhakikisha haki inatolewa kwa pande zote katika mizozo inayo-husiana na wafanyakazi,” akasema Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

# Wanafunzi wapewe ujuzi kuambatana na hali ya soko la ajira - Katibu Mkuu

NA SAMUEL WAITITU, KNA

**K**atibu Mkuu ka-tika wa Elimu ya Juu na Utafiti, Dkt. Beatrice Inyan-gala, amesisitiza haja ya kutayarisha wanafunzi kwa ulimwengu wa kazi unaobadilika. Ali-sisitiza kwamba taasi zinapaswa kusaidia wanafunzi kuzinga-tia mawazo ya kina, kubadilika, na ubunifu, badala ya kukariri uk-weli tu.

Alikuwa akizung-umza katika Chuo Ki-kuu cha Embu wakati wa Wiki ya Utumishi ya kila mwaka, am-bayo ililenga kusaidia wanafunzi kupata ush-auri na mwongozo.

Katibu Mkuu alisema kuwa soko la ajira lin-abadilika kwa kasi kutokana na maen-deleo ya kiteknolojia na mitambo ya kisasa, inayohitaji watu bin-afsi kuendelea kus-asishkua ujuzi wao ili kubaki muhimu katika soko la ajira. “Kwa sasa, tuko ka-tika mapinduzi ya nne ya viwanda ambapo mambo yanabadilika kwa kasi na ulimwengu wa kazi unaongozwa na teknolojia, mtandao wa mambo, teknolo-jia ya blockchain, uk-

weli wa mtandaoni na uliodhabitiwa,” akasema.

Hili, alisema, lina-hitaji wanafunzi kuji-panga upya ili kupata ujuzi unaohitajika am-bao utawasaidia kuk-abiliana na ulimwengu unaoendeshwa na te-knolojia. “Twataka wanafunzi wakitoka chuo kikuu wafikirie zaidi ya ulimwengu wa ajira jinsi wanavyoweza kutengeneza fursa za kuajiri wengine,” akasema.

Alisema idara yake inafanya kazi kwa karibu na vyuo vi-kuu ili kutangaza na kutekeleza programu zinazosaidia vijana ku-ingia kazini kwa ma-fanikio. Kutimiza hilo, Dkt. Inyangala alisema serikali itaimarisha mitandao ya wanafunzi wa vyuo vikuu ili ku-wasaidia kujenga mitaji ya kijamii ambayo ita-wapa fursa huko nje.

Katibu Mkuu al-iongeza kwamba, katika jitihada za kui-marisha daraja kati ya vyuo vikuu na sekta ya ajira, serikali in-ashughulikia moti-sha ambayo inaweza kuwezesha viwanda kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi kupata ujuzi wa vitendo.



**KENYA VETERINARY BOARD**

Upholding Veterinary Standards

## PRE-QUALIFICATION/REGISTRATION OF SUPPLIERS

**TENDER NUMBER**

**KVB/ONT/01/2024-2025**

**PRE-QUALIFICATION /REGISTRATION OF SUPPLIERS FOR SUPPLY/ PROVISION OF GOODS, WORKS AND SERVICES FOR THE FINANCIAL YEARS 2024/2025 - 2025/2026**

Kenya Veterinary Board (KVB) under the State Department for Livestock P.O. Box 513-00605 Uthiru invites applications for pre-qualification of suppliers and tenders from interested and eligible bidders for the following goods, services and works for the financial years 2024/2025 - 2025/2026.

Tender documents containing detailed requirement can be downloaded free of charge from our website: [www.kenyavetboard.or.ke](http://www.kenyavetboard.or.ke) and the Public Procurement Information Portal [PPIP] [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke). All clarification/ amendments will be published on Kenya Veterinary Board website and tenderers are required to regularly check for any addendums or amendments in the course of the bidding periods prior to the closing date.

The completed bids in plain sealed envelope marked with tender reference number and tender name shall be deposited in tender box located at Kenya Veterinary Board Head Quarters, P.O. Box 513-00605 Uthiru on 25<sup>th</sup> February, 2025 at 10.00am.

Tenders shall be opened immediately thereafter in the presence of bidders' representatives who wish to attend at the KVB headquarters Upper Kabete, Veterinary Laboratories.

Dr. Mary T. Agutu,  
CHIEF EXECUTIVE OFFICER,  
KENYA VETERINARY BOARD.



## JOB ADVERTISEMENT

Our esteemed client, a leading financial institution is committed to enhancing efficiency and effective service delivery. To support this mission, we are seeking dynamic, innovative, and experienced individuals to join the team

| Position                                   | Department               |
|--------------------------------------------|--------------------------|
| Head of Risk and Compliance                | Risk & Compliance        |
| Head of Retail & SME                       | Retail & SME             |
| Company Secretary & Head of Legal Services | Legal                    |
| Head of Human Resources                    | Human Resources          |
| Head of Credit Management                  | Credit Management        |
| Head of Finance & Administration           | Finance & Administration |

View the detailed job descriptions here: <https://tinyurl.com/4kw5zp78>

Interested and qualified individuals are invited to submit their applications to [applyjobs@cdl.africa](mailto:applyjobs@cdl.africa) using the job title as the email subject. Enclose copies of academic and professional certificates, a detailed CV highlighting work experience, and provide the names and addresses of three referees. Include your current and expected salaries, allowances, and benefits. Applications should reach us by **25<sup>th</sup> February 2025**.

**NB: Our Client is an equal opportunity employer and only shortlisted candidates will be contacted.**

# Shirika la Reli Kenya larudia mradi wa reli ya mjini Mombasa huku likitenga Sh1.1b za fidia

**NA SADIK HASSAN, KNA**  
Shirika la Reli la Kenya (KRC) limezidisha juhudi za kuanzisha treni ya kuhudumu kati ya kituo cha Reli ya Standard Gauge (SGR) na Kituo Kikuu cha Reli kilicho ndani ya mji wa Mombasa.

Mradi huo wa thamani ya Sh4.2 bilioni, ambao ulianza Septemba 2022, ulikatiwa na changamoto za kutwaa ardhi na ukasitishwa ukiwa umefikia asilimia 65 kukamilika.

Hata hivyo, tangu wakati huo Wizara ya Uchukuzi imetenga Sh1.1 bilioni kwa Tume ya Kitaifa ya Ardhi ili kuanza kufidia eneo hilo la kilomita 1.4, na hivyo kufungua njia ya ukarabati wa Reli ya Meter Gauge (MGR) Mombasa hadi Miritini.

Mradi huo utakapoka-



**Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Kenya Bw. Philip Maingi (kushoto) na mwenzi wakikagua kazi katika kituo cha reli kilicho ndani ya mji wa Mombasa.**

milika, abiria wanaotumia huduma ya abiria ya Madaraka Express na stesheni saba kando ya Reli ya SGR, wanaofika au kuondoka Mombasa, watatumia njia ya Reli ya Meter Gauge (MGR) kufika kituo cha eneo la katikati mwa mji

wa Mombasa. Sehemu ya pili ya mradi huo inahusisha ukarabati wa Kituo Kikuu cha Reli cha Mombasa na ujenzi wa vituo vinne vidogo vya Changanwe Mashariki, Changanwe Magharibi, Miritini na Shimanzi.



**Sehemu ya Reli ya kawaida ambayo itaunganishwa na reli ta SGR kutoka kituo cha SGR cha Mombasa hadi kituo cha reli kilicho ndani ya mji wa Mombasa.**

Mradi huu pia unahusu ujenzi wa daraja la watu wanaotembea linalounganisha jukwaa la SGR na MGR, sehemu ya kugeuza treni na daraja la reli yenye urefu wa mita 480 kuvuka barabara ya Makupa

Causeway.

Treni hiyo ya abiria itawawezesha wakazi wa Mombasa kuwa na njia mbadala ya usafiri hivyo basi kupunguza mson-gamano kwa usafiri wa barabarani.

Reli hiyo ya abiria ni sehemu ya Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka (MRT) unaotekelezwa na Wizara ya Barabara na Uchukuzi, ukiwemo Mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) ili watu wasafiri kwa usalama na ufanisi.

Mkurugenzi Mkuu wa KRC Bw Philip Mainga alisema kuwa mradi huo uko katika hatua ya juu ya ujenzi na watumiaji wa treni hivi karibuni watafurahia usafiri kati ya kituo cha SGR Miritini na eneo la katikati mwa mji wa Mombasa.

“Tunatazamia kuanzisha treni hiyo katika Kaunti ya Mombasa hivi karibuni. Ikianza kazi, wakazi, watalii na wapenda treni hadi Mombasa watatumia treni hiyo. Treni hiyo itarahisisha usafiri sio tu kwa kituo cha Mombasa mjini bali pia maeneo yaliyo kati ya mji huo,” akaongeza Mkurugenzi huyo Mkuu wa Shirika la Reli Kenya.



## INVITATION TO TENDER

Kenya Power invites tenders from interested bidders for provision of the following:-

| NO. | TENDER NO.                | ITEM DESCRIPTION                                                                                                                                                                                                               | TENDER COMMENCEMENT DATE | PRE BID MEETING                                                                                                                                                                                                                     | TENDER CLOSING DATE                |
|-----|---------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|------------------------------------|
| 1.  | KP1/9A.3/OT/15/24-25      | Procurement of Distribution Network Fault Indicators                                                                                                                                                                           | Thursday 13.02.2025      | N/A                                                                                                                                                                                                                                 | Thursday 06.03.2025 at 10.00 a.m.  |
| 2.  | KP1/9A.2/OT/023/ICT/24-25 | Upgrade from Tape Backup to Disk-Based Long-Term Retention (LTR) Appliance for Enterprise Data Backup Environment                                                                                                              | Thursday 13.02.2025      | N/A                                                                                                                                                                                                                                 | Thursday 27.02.2025 at 10.00 a.m.  |
| 3.  | KP1/9A.2/OT/024/ICT/24-25 | Procurement of Spares for Substation Automation and RTU                                                                                                                                                                        | Friday 14.02.2025        | N/A                                                                                                                                                                                                                                 | Friday 28.02.2025 at 10.00 a.m.    |
| 4.  | KP1/9A.2/OT/027/ADM/24-25 | Provision of Cleaning Services Company-wide for General Bidders                                                                                                                                                                | Thursday 13.02.2025      | Tuesday 18.02.2025 at 10.00 a.m. (Stima Plaza, Auditorium)                                                                                                                                                                          | Wednesday 05.03.2025 at 10.00 a.m. |
| 5.  | KP1/9A.2/OT/028/ADM/24-25 | Provision of Cleaning Services Company-wide for YWPWD                                                                                                                                                                          | Thursday 13.02.2025      | Tuesday 18.02.2025 at 10.00 a.m. (Stima Plaza, Auditorium)                                                                                                                                                                          | Wednesday 05.03.2025 at 10.00 a.m. |
| 6.  | KP1/9A.2/OT/030/LS/24-25  | Repair of 2no. Microfilm Scanner and 2no. Documents Scanner for the Record Management Section: Repair & Maintenance of 4no. Electronic Mobile Shelving Units for the Records Management Section and Corporate Heritage Section | Thursday 13.02.2025      | <b>Mandatory Pre-Bid/Site Meeting</b><br>Thursday 20.02.2025 9.00 a.m. – 9.30 a.m.<br>9.30 a.m. – 10.15 a.m. (Stima Plaza 7th Floor Nairobi)<br><br>10.45 a.m. – 11.30 a.m. (Electricity House 5 <sup>th</sup> Floor Harambee Wing) | Wednesday 26.02.2025 at 10.00 a.m. |

Tender documents detailing the requirements of the above tenders may be obtained from the Kenya Power website ([www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke)) from the dates shown above.

**GENERAL MANAGER  
SUPPLY CHAIN & LOGISTICS**

[www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke)

DIAL \*977# | Access Kenya Power services fast and easy

[www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke) | [Customer@kplc.co.ke](mailto:Customer@kplc.co.ke) | Kenya Power | [KenyaPower](https://www.facebook.com/KenyaPower) | 97771 | 020-020 705, 0752-190 119



## Salaries & Remuneration Commission



## ADVERTISEMENT OF VACANT POSITIONS

The Commission seeks to recruit qualified and competent persons to fill the following vacant positions.

| Position                                              | Job Grade | Number of Positions |                  |
|-------------------------------------------------------|-----------|---------------------|------------------|
| Deputy Director - Collective Bargaining Negotiations  | RL3       | 1                   | Re-advertisement |
| Deputy Director - Performance and Productivity        | RL3       | 1                   |                  |
| Head of Information Communications Technology - ICT   | RL3       | 1                   |                  |
| Principal Officer, Human Resources and Administration | RL4       | 1                   | Re-advertisement |
| Principal Officer, Collective Bargaining Negotiations | RL4       | 1                   | Re-advertisement |
| Principal Officer, Performance and Productivity       | RL4       | 1                   |                  |
| Principal Legal Officer                               | RL4       | 1                   |                  |
| Senior Officer, Collective Bargaining Negotiations    | RL5       | 2                   | Re-advertisement |
| Senior Officer, Research, Monitoring and Evaluation   | RL5       | 1                   |                  |
| Senior Officer, Allowances and Benefits               | RL5       | 1                   | Re-advertisement |
| Senior Officer- Supply Chain Management               | RL5       | 1                   |                  |
| Knowledge Management Officer                          | RL6       | 1                   |                  |
| Driver (2)                                            | RL8B      | 2                   |                  |

### APPLICATION PROCESS

- Interested and qualified persons are requested to register and apply to the **SRC E-recruitment Portal**. Details of the positions are in the Commission website under Career Section.
- All applications should be uploaded together with detailed Curriculum Vitae, a copy of ID/Passport, copies of academic certificates, testimonials and any other relevant supporting documents. Hard copies and email applications shall not be considered.
- Those who might have applied for the re-advertised positions are encouraged to re-apply.
- Successful candidates **MUST** submit all clearances in relation to Chapter six before onboarding.

The Commission is an equal opportunity employer and the Marginalized and Persons with disabilities are encouraged to apply. Only Shortlisted candidates will be contacted.

The application letter should be addressed to:

**THE COMMISSION SECRETARY/CEO  
Salaries & Remuneration Commission  
Williamson House, 6th Floor  
4th Ngong Avenue,  
P.O Box 43126-00100 NAIROBI.**

To be received on or before **26th February, 2025**



# Waziri asema huduma zitaendelea licha ya Amerika kuondoa msaada

NA EMMANUEL MBUTHIA  
NA CLINTON NG'IELA, KNA

Waziri wa Afya (CS) Dkt. Deborah Barasa amesema kuwa Wizara ya Afya (MoH) itachukua hatua zote zinazohitajika ili kupunguza athari za kuondolewa kwa msaada wa Amerika.

Akizungumza katika kikao na wanahabari jijini Nairobi, Dkt Barasa alisisitiza umuhimu wa kufikiria kuhusu suluhu endelevu za ufadhili wa afya nchini. Alisisitiza haja ya kuimarisha Mamlaka ya Afya ya Jamii (SHA), ambayo itafadhiliwa kupitia michango ya wanachama, Hazina ya Kitaifa, na vyanzo vingine vya ufadhili.

Waziri alihakikisha kwamba mkakati huo utahakikisha kuendelea kutoa huduma na matibabu kwa wagonjwa walio na Virusi vya Ukimwi, TB na Malaria ambao hapo awali walipokea msaada kutoka kwa serikali ya Amerika.

“Licha ya changamoto za afya duniani, tunataka kuwahakikishia kwamba Serikali ya Kenya, kupitia Wizara ya Afya, itahakiki-



Waziri wa Afya Dkt. Deborah Barasa, akihitubia wanahabari mnamo Jumatano Februari 5 katika jumba la Afya House, Nairobi, wakati wa taarifa ya kila wiki kwa vyombo vya habari kuhusu Taifa Care, ambapo aliahidi kuendelea kwa huduma za afya licha ya changamoto zilizopo.

sha uendeleu wa huduma muhimu za afya kwa Wakenya wote, ikiwemo kwa wagonjwa HIV, TB, na huduma nyingine muhimu za afya,” akasisitiza Barasa.

“Kuondolewa kwa

**Kuondolewa kwa ufadhili ni tahadhari kwa Wakenya kuzingatia zaidi uendeleu-Kati-bu Mkuu**

fedha hizo ni tahadhari kwetu Wakenya kuzingatia uendeleu, jinsi tunavyoweza kusimama kwa miguu yetu wenyewe, na jinsi tunavyoweza kujitegemea katika masuala ya afya,” akasema. Waziri pia alitambua wajibu ambao washirika wa kimataifa, likiwemo Shirika la Afya Duniani (WHO), Mpango wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa kuhusu HIV (UNAIDS), miongoni mwa mengine, wameitimiza katika masuala ya ushauri wa kiufundi na

uongozi katika sekta ya afya.

Mkurugenzi Mkuu wa Afya, Dkt. Patrick Amoth alisisitiza umuhimu wa kufanya kazi na wadau wote, yaani, serikali za kaunti na washirika wote wa maeendeleo, ili kujumuisha huduma za afya.

“Huduma za msingi za afya kwa kawaida huunganishwa, ni za kina, zinakuza ushirikishwaji na hiyo ndiyo njia ya kufuata tunapotekeleza Huduma ya Taifa,” akaongeza Amoth.

Aliungama kwamba Wizara ya Afya imejifunza somo kutoka kwa kaunti ambazo zimetekeleza mbinu bora na akatoa wito kwa kaunti zingine zibadilishane uzoefu wao, ili waweze kuunganisha huduma za afya kwa pamoja. “Tunaposhughulikia suala la kutafuta rasilimali za ndani, ni muhimu kukagua michakato yetu ili kuhakikisha kuwa tunaweza kufadhili programu zetu kikamilifu,” akasema.

Dkt. Amoth aliahidi kuwa Wizara ya Afya itaendelea kutoa taarifa ya kina ya kila wiki kuhusu sekta ya afya.

## Chombo cha angani kuboresha ujenzi katika makao duni



NA EDITH MUPA  
(PCO)

Mradi wa Pili wa Kuboresha Mitaa ya Mabanda Kenya (KISIP2) umewahimiza watafiti chipukizi kumbatia teknolojia za kisasa za kidijitali ili kuimarisha ujuzi na umahiri wao katika kushughulikia mipango ya ujenzi nchini.

Akizungumza katika Taasisi ya Kenya ya Kuchunguza na Kuchora Ramani eneo la Ruaraka, Nairobi, wakati wa hafla ya kukabidhi ndege ndogo aina ya Matrice RT 350 Series Drones, Mratibu wa Mradi wa Kitaifa wa KISIP2 George Arwa alisema kuwa ndege hizo zisizo na rubani za LiDAR Technology “ni nyongeza muhimu kwa

zana zitakazoimarisha juhudi za uchunguzi na uchoraji wa ramani kote nchini Kenya.”

“Drones hizi zina vifaa vya teknolojia ya kisasa iliyoundwa ili kutoa data ya usahihi wa juu kupitia mifumo yao ya RTK na LiDAR,” akasema Arwa.

“Lengo la msingi ni kusaidia Idara ya Utafiti katika kufanya tafiti kwa ufanisi na kuchora ramani ya taifa, kwa kuzingatia hasa mitaa ya mabanda ambayo KISIP2 inajitahidi kuboresha,” akaongeza.

Mratibu huyo pia alisema Idara ya Serikali ya Nyumba na Ustawi wa Miji imepata ufanisi mkubwa kupitia michakato ya kidijitali.



## MASINDE MULIRO UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

Tel, 0572505222/3 or 0733120020/2 or 0702597360, P.O. BOX 190 – 50100 Kakamega, Kenya,  
Email: [info@mmust.ac.ke](mailto:info@mmust.ac.ke); [procurementofficer@mmust.ac.ke](mailto:procurementofficer@mmust.ac.ke), Website: [www.mmust.ac.ke](http://www.mmust.ac.ke)

### TENDER NOTICE

Masinde Muliro University of Science and Technology hereby invites eligible and interested contractors to tender for the following Tenders:

| SN | TENDER NUMBER           | TENDER NAME                                                                                             | BID SECURITY IN KSHS. | ELIGIBILITY |
|----|-------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------------------------|-----------------------|-------------|
| 1  | MMUST/ECE/006/2024-2025 | Supply, Installation, Testing And Commissioning Of Electrical Engineering Teaching Laboratory Equipment | 400,000               | Open        |
| 2  | MMUST/EST/007/2024-2025 | Proposed Renovation & Extension of MMUST Clinic                                                         | 400,000               | Open        |

Interested and eligible firms may obtain further information from procurement office during normal working hours. Tender documents may be viewed and downloaded **FREE** of charge from the University website: [www.mmust.ac.ke](http://www.mmust.ac.ke) or PPIP Portal <https://www.tenders.go.ke>

Duly completed tender documents enclosed in plain sealed envelopes clearly marked with Tender name and Number shall be sent to;

**Vice Chancellor  
Masinde Muliro University of Science and Technology- MMUST  
P. O. Box 190-50100  
Kakamega**

Or, dropped in the Tender Box situated at the main entrance of the Administration Block (ABA) Building at Masinde Muliro University of Science & Technology (MMUST) main campus along Kakamega – Webuye Road in Kakamega and not any other place so as to reach the University not later than 10:00am on **Tuesday 4<sup>th</sup> March, 2025**. Opening of the bid documents will be done immediately thereafter in the presence of applicants or their representatives who choose to attend.

**Vice Chancellor  
Masinde Muliro University of Science & Technology**



## TENDER NOTICE

Kenya Electricity Transmission Company Limited (KETRACO) is a State Corporation whose mandate is to plan, design, construct, operate, own, and maintain high voltage national electricity transmission grid and regional power interconnectors.

KETRACO now invites tenders from interested/eligible firms to bid for the tender given below:

| S/no | Tender Description                                                                                                                   | Tender Reference Number | Closing Date                       |
|------|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------|------------------------------------|
| 1.   | Tender Document for Provision of Insurance Brokerage Services for General & Group Life Classes of Insurance for the Period 2025-2027 | KETRACO-PT-001-2025     | 6th March 2025 at 10:30 am EAT     |
| 2.   | Procurement of Spares for Emergency Replacement for Pole 2 Valve Equipment at Suswa Converter Station.                               | KETRACO-PT-002-2025     | 11th March 2025 as at 10:30 am EAT |
| 3.   | Procurement Scada Equipment.                                                                                                         | KETRACO-PT-003-2025     | 5th March 2025 as at 10:30 am EAT  |

KETRACO tenders run on SAP ARIBA e-procurement platform and therefore the tender document detailing the requirements may be viewed by clicking on the link provided in KETRACO website ([www.ketraco.co.ke](http://www.ketraco.co.ke))

All enquiries on this tender should be channeled through [kettenders@ketraco.co.ke](mailto:kettenders@ketraco.co.ke) ; cc [hkiser@ketraco.co.ke](mailto:hkiser@ketraco.co.ke) or through message board in SAP Ariba.

Complete tender documents shall be electronically submitted through SAP ARIBA platform on or before the dates as indicated in the table above for specific tenders.

|------------|-------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------|----------------------|
| 1000001276 | Construction of Kiunga Power Station Hesco Bastion Wall.                | 500,000.00                                                        | 13.03.2025@10.00am   |
| 1000001283 | Tender for Supply and Delivery of Composite Poles-Open to Manufacturers | Lot 1: 3,000,000.00<br>Lot 2: 3,000,000.00<br>Lot 3: 3,000,000.00 | 03.03.2025 @10:00am  |

- Tendering will be conducted under open competitive method (National) using a standardized tender document. Tendering is open to all qualified and interested Tenderers.
- Qualified and interested tenderers may obtain further information and inspect the Tender Documents during office hours **8.00am - 12.45pm to 1.45pm-4.00pm Monday to Friday** in Rural Electrification and Renewable Energy Corporation Offices situated in Kawi Complex, Block C, Ground floor.
- A complete set of tender documents may be viewed and downloaded by interested tenderers free of charge electronically from the Website [www.rerec.co.ke](http://www.rerec.co.ke) under tender documents or through the e-procurement portal using <https://suppliers.rea.co.ke:44300/irj/portal> and on the Public Procurement Information Portal <https://tenders.go.ke>.
- Tender documents may be viewed and downloaded for free from the website [www.rerec.co.ke](http://www.rerec.co.ke). Tenderers who download the tender document must forward their particulars immediately to [tenders@rerec.co.ke](mailto:tenders@rerec.co.ke) to facilitate any further clarification or addendum.
- Tenders shall be quoted in Kenya Shillings and shall include all taxes. Tenders shall remain valid for 147 days from the date of opening of tenders.
- All Tenders must be accompanied by a tender Security in form of a bank guarantee as indicated in the TDS. Original of the tender security must be deposited to the tender box described in this document.
- The Tenderer shall chronologically serialize all pages of the tender documents submitted.
- Completed tenders must be delivered to Rural Electrification and Renewable Energy Corporation electronically through <https://suppliers.rea.co.ke:44300/irj/portal> on or before the date and time indicated above.
- Only Electronic Tenders will be permitted.
- Tenders will be opened immediately after the deadline date and time specified above or any dead line date and times specified later. Tenders will be publicly opened in the presence of the Tenderers' designated representatives who choose to attend at the address below.
- Any addendum to this tender shall be uploaded to the Corporation's website [www.rerec.co.ke](http://www.rerec.co.ke) under tender documents.
- Late tenders will be rejected.
- The addresses referred to above are:

### Address for obtaining further information on tender documents

For hand Courier, Original Bid security delivered to the tender Box (Kawi Complex, Block C, Ground floor, Off Popo Road,). Contact Manager, Supply chain management, telephone number: 0709193000 and e-mail address: [tenders@rerec.co.ke](mailto:tenders@rerec.co.ke)

**Address for Submission of Tenders:** Online Through <https://suppliers.rea.co.ke:44300/irj/portal>

**Address for Opening of Tenders. Kawi Complex, Block C, Ground floor, online system**

Original Bid security delivered to the tender Box (Kawi Complex, Block C, Ground floor, Off Popo Road,). Contact Manager, Supply chain management, telephone number: 0709193000 and e-mail address: [tenders@rerec.co.ke](mailto:tenders@rerec.co.ke)

**Address for Submission of Tenders:** Online Through <https://suppliers.rea.co.ke:44300/irj/portal>

**Address for Opening of Tenders. Kawi Complex, Block C, Ground floor, online system**

**Name:** Dr. Rose N. Mkalama  
**Designation:** CHIEF EXECUTIVE OFFICER

**Signature:**.....  
**Date:** 06.02.2025



# Serikali yazindua mpango wa miaka 5 kufufua kilimo cha unyunyizaji kwa usalama wa chakula

NA IAN CHEPKUTO, KNA

Serikali inaandaa mpango mkakati wa miaka mitano wa kufufua sekta ya kilimo cha unyunyizaji na kuhakikisha usalama wa chakula nchini.

Katibu Mkuu wa Idara ya Unyunyizaji, Ephantus Kimotho, amesema Mpango wa Kitaifa wa Uwekezaji Katika Sekta ya Unyunyizaji (NISIP) kwa sasa unashirikisha umma kote nchini huku akielezea mwongozo wa kufikia uwezo wa kilimo nchini, hasa katika Maeneo Kame na Nusu Kame (ASAL).

Akihutubia warsha ya mashauriano kuhusu Mpango wa Kitaifa wa Uwekezaji Katika Sekta ya Unyunyizaji (NISIP) jijini Nairobi, Kimotho alitangaza kwamba ushirika huo unaoendelea wa umma ukihusisha wadau mbalimbali, ni hatua ya kuelekea kuzinduliwa rasmi kwa mpango mkakati huo, ambao umepangwa kufanyika Machi 21 mwaka huu.

Baadhi ya wadau wali-ohusika katika mchakato huo ni pamoja na taasisi za fedha, wauzaji wa teknolojia ya kilimo, wakulima, na wasomi, miongoni mwa wengine.

Katibu Mkuu alisema kuwa mpango huo wa unyunyizaji unaambatana na nguzo ya maendeleo ya serikali, Agenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi ya Bottom-Up (BETA), ambayo inalenga mabadiliko katika sekta ya kilimo ili kushughulikia usalama



**Waziri wa Unyunyizaji Ephantus Kimotho, akihutubu wakati wa warsha kuhusu Mpango wa Uwekezaji Katika Sekta ya Kitaifa ya Unyunyizaji (NISIP) iliyofanywa katika Boma Hotel, Nairobi.**  
PICHA: BENEDICT WASICHE.

wa chakula na kutengeneza ajira. “NISIP inataka kushughulikia changamoto za maji tulizonazo katika sekta ya kilimo na kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa, hasa ukame na mafuriko, ili kuhakikisha kuendelea kwa uzalishaji katika ASAL. Ndiyo maana unyunyizaji, ambao ni ki-

pengele muhimu katika kusaidia BETA, ni muhimu sana katika kuhakikisha tija endelevu,” akasema.

Katibu Mkuu alisema NISIP inakusudia kuongeza matumizi ya ardhi iliyo chini ya unyunyizaji hadi zaidi ya ekari milioni moja ifikapo 2030, kupitia kuwekeza zaidi katika uvunaji wa maji, mabwawa ya kuhifadhi maji, na kuboresha miundomsingi ili kushughulikia mahitaji ya haraka na uendelevu wa muda mrefu.

Kuhusu ustahimilivu wa tabianchi, Kimotho alisema mpango huo unalenga kushughulikia mahitaji ya haraka na yajayo kwani utatayarisha nchi kuweka vipaumbele vya uendelevu na kuweka mkakati mipya ya kilimo.

Alisema kuwa zaidi ya asilimia 80 ya ardhi ya Kenya iko chini ya ASAL na ina uwezo mkubwa wa

kilimo ambao, ukitumiwa kikamilifu utakabiliana na uhaba wa chakula na kupunguza utegemezi kupita kiasi wa uagizaji bidhaa kutoka nje.

Akaongeza: “Kwa kupunguza uagizaji wa chakula, Kenya itaunda nafasi nyingi za kazi, kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni, kuwezesha gharama ya chini ya maisha, na kuimarisha uchumi wa nchi,” akasema.

Katibu Mkuu alifanua kuwa Mpango wa NISIP una hatua tano

**Mpango wa TNISIP una hatua tano muhimu za uwekezaji katika kuboresha kilimo cha unyunyizaji-Kimotho**

muhimu za uwekezaji kwa ajili ya kuimarisha kilimo cha unyunyizaji.

Alitaja hatua hizo kuwa kupanua ardhi ya unyunyizaji, ushirikishwaji wa hali ya juu na wahusika wakuu katika sekta binafsi, mashirika yasiyo ya faida, na washirika wa maendeleo ili kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo kuelekea kufikia kilimo cha unyunyizaji kinachohimili mabadiliko ya tabianchi.

Kimotho aliongeza kuwa Mpango wa NICIP utashirikiana na kampuni za biashara ya kilimo na wakulima wakubwa walio tayari kukodisha ardhi inayomilikiwa na serikali kwa ajili ya kilimo, kuangalia uwezekano wa pembejeo za kilimo zinazotolewa kwa ruzuku kama vile pampu za kawaida na za jua, pamoja na kuwezesha wakulima kupata soko la ndani na nje ya nchi.

Katibu Mkuu alisema kuwa changamoto kuu katika eneo la ASAL ni upatikanaji wa vyanzo endelevu vya maji, akiongeza kuwa uwekezaji katika uvunaji wa maji kama vile uwekaji wa mapipa ya maji na uchimbaji visima utapunguza ukosefu wa maji na malisho kwa mifugo na matumizi ya nyumbani. Alibainisha kuwa ukosefu wa usalama umechangiwa na uhaba wa malisho na maji.

Akasema: “Changamoto kubwa katika kaunti za ASAL ni maji. Mpango huo utakabiliana na uhaba wa chakula kupitia mi-

kakati kama vile kujenga mabwawa, vidimbwi vya maji na hifadhi.

Aliongeza kuwa, kwa muda mrefu, mpango huo unalenga kutatua migogoro, kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, na kuendeleza kuisi pamoja kwa amani, na hatimaye kukuza uchumi imara.

Kimotho alibainisha kuwa, katika kutimiza lengo la jumla la Mpango wa Taifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Unyunyizaji (NISIP), kuna haja ya ushirikiano wa karibu chini ya mipango ya Ushirika kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) na washirika wa maendeleo, wazalishaji na wauzaji wa teknolojia ya unyunyizaji.

“Kwa kutekeleza asilimia 50 ya matarajio yaliyoainishwa katika NISIP, tunaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa uagizaji wa chakula kwa asilimia 50. Na kwa kutekeleza asilimia 100, tutapunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje kwa karibu sufuri,” akasema.

Akaongeza: “Kupitia hili, tutakuwa tunatengeneza ajira zaidi, kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, kukuza mapato na kuongeza mapato ya serikali.”

Wakati huo huo, Katibu Mkuu alisema wahusika wengine muhimu wanahitaji kuingizwa, haswa walio katika suluhisho la kilimo kinachozingatia mabadiliko ya hali wakulima wa mikataba na uwekezaji wa mitaji ya kibinafsi.

## Mpango wa KALRO wa kukagua mchanga kidijitali kuboresha mbinu za kilimo kwa kaunti 45

NA KIPTANUI CHERONO (KNA)

Shirika la Utafiti wa Kilimo na Mifugo Kenya (KALRO) limezindua mpango wa kitaifa wa kukagua udongo kidijitali ili kutathmini rutuba ya udongo kote nchini.

Kulingana na Bi Agnes Yobterik, afisa wa usimamizi wa mazingira na rasilimali katika KALRO, mpango huo wa kitaifa wa utatekelezwa katika kaunti 45, isipokuwa kaunti za Nairobi na Mombasa.

Mpango huo, alisema, unalenga kuendeleza mfumo wa taarifa za

udongo. Aliongeza kuwa uchanganuzi wa rutuba ya udongo utafanywa ili kutathmini hali ya udongo kutoka sehemu 77,969 zilizolengwa za sampuli kote nchini.

Akizungumza wakati wa kikao na wanahabari mjini Eldoret, ambapo timu kutoka KALRO itakuwa ikiendesha shughuli hiyo kwa ushirikiano na serikali za kaunti za Uasin Gishu, Elgeyo-Marakwet, Trans Nzoia, Turkana, na Bungoma, Bi Yobterik alisema kuwa uamuzi wa kutekeleza mpango huo ulichochea na changamoto kuhusiana na rutuba ya udongo zina-

zokumba nchi.

“Mpango kadhaa imefanywa hapo awali ili kulewa hali ya udongo wetu, lakini datatakwimu hizo ni zaidi ya miaka 10, tafiti chache zilizofanywa katika kipindi cha kati zimeonyesha kuwa udongo katika maeneo mengi ya kilimo umebadilika,” akasema Bi Yobterik.

Kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa wa kuangalia upya hali ya udongo wetu ili tujue kiwango cha virutubisho mbalimbali ili kuweza kuongoza kuhusu namna ya kutumia mbolea.

Alisema, watapendekeza kwamba mbolea



**Maafisa wakichukua sambuli za udongo kukaguliwa kutoka Kaunti Ndogo ya Moiben.**

yoyote itakayotengenezwa itengenezwe kulingana na mahitaji ya kilimo.

Bi Yobterik aliongeza kuwa lengo la mpango huo ni nchi kuelewa udongo wake, hasa mahitaji ya virutubisho, na matumizi ya mbolea iliyotengene-

zwa mahususi.

Katika maelezo yake, Naibu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Chakula ya KALRO Kitale, Dkt. Mary Koech, alisema wanatarajia kwamba kufikia mwisho wa shughuli hiyo

watakuwa wamejua hali ya rutuba ya udongo katika maeneo mbalimbali na kutoa mapendekezo maalumu ya mbolea kwa wakulima.

Aliongeza kuwa Kalro inatarajia kuwa matokeo ya shughuli hiyo yatafahamisha watunga sera kuhusu matumizi ya mbolea nchini na kufahamisha serikali kuhusu usambazaji wa baadaye wa mbolea ya ruzuku.

“Serikali itajua ni eneo gani linakosa madini ya udongo, na aina ya mbolea inayofaa kwa eneo gani, kati ya haya yote tunatarajia tutaboresha uzalishaji na kuhakikisha tuna uhakika wa chakula cha kutosha nchini,” Dkt. Koech alisema.

Kuhakikisha ufanisi na wa mpango huo, vijana wameteuliwa kusaidia katika kukusanya sampuli za udongo.

# Misri na Kenya zaimarisha ushirikiano wa biashara, diplomasia na amani katika eneo

Ziara ya hivi majuzi ya Mtukufu Rais William Samoei Ruto mjini Cairo ili iadhimisha ziara ya kwanza ya kitaifa ya Rais wa Kenya na kuadhimisha miongo sita ya uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi hizo mbili. Ziara hiyo ilihusisha kutiwa saini kwa mikataba kadhaa ya mashauriano ya kisiasa, ushirikiano wa uwekezaji na maendeleo endelevu.

Uhusiano wa Kenya na Misri ulianza kabla ya ukoloni, ukiwezesha na njia za biashara zinazounganisha Afrika, Mashariki ya Kati, Ulaya na Asia. Kuwepo kwa Misri kando ya Mto Nile na uwezo wa Kenya wa kutumia Bahari ya Hindi kumeweka mataifa hayo mawili kama washiriki muhimu katika biashara ya kale na mabadilishano ya kitamaduni.

Misri na Kenya zina-shiriki zaidi ya ukaribu wa kijiografia na dhama ya milele kwa bara la Afrika. Mataifa hayo mawili pia yalishiriki ana kufikia maono yao ya pamoja ya Afrika isiyo na ukoloni. Inajulikana kuwa Misri iliunga mkono harakati za kupigania uhuru wa Kenya mara kadhaa. Zaidi ya



NA DKT. MUSALIA MUDAVDI NA DKT. BADR ABDELATTY



hayo, “Sauti ya Afrika,” idhaa ya kwanza ya radio kutangaza kwa Kiswahili, ilizinduliwa mjini Cairo. Viongozi kama vile Oginga Odinga, Tom Mboya, na James Gichuru walikimbilia Misri, huku baadhi yao wakipewa hati za kusefiria za kidiplomasia za Misri ili kukuza uhuru wa Kenya duniani baada ya wakoloni kufuta hati zao za kusafiria.

Msaada wa Misri kwa ukombozi wa Kenya haukuhusisha serikali yake tu. Kanisa la Kiorthodoksi la Alexandria pia lilitetea uhuru wa Kenya, huku makasisi katikwa Kanisa la Holy See of St. Mark wakizuilwa kwa kutoa mahubiri ya kupinga ukoloni. Chama cha KANU na

Chama cha KADU vilifungua ofisi zake mjini Cairo katika kipindi hicho. Kwa kuzingatia historia hii, inaeleweka ni kwa nini Kenya ilichagua kuanzisha ofisi yake ya kidiplomasia mjini Cairo punde tu baada ya uhuru, nafasi ya pili baada ya ubalozi wake mjini London.

Katika miongo sita iliyopita, mshikamano wa pande hizi umeunda uhusiano kati ya

**Misri na Kenya zina-shirikiana kutekeleza Ajenda ya 2063 ya Jumuiya ya Afrika**

Nairobi na Cairo. Licha ya changamoto kama vile ugaidi, ukosefu wa amani na mabadiliko ya hali ya hewa, mataifa hayo mawili yanaendelea kufanya kazi pamoja kushughulikia vipaumbele vya kisiasa vya kienyeo, kuendeleza utulivu na maendeleo ya bara, na kutumikia maslahi ya Afrika na Kusini mwa Ulimwengu. Pia yanashirikiana kukuza maendeleo shirikishi ya kiuchumi, amani na utulivu kote barani Afrika. Nchi zote mbili zina maono ya umoja wa Afrika, zikijitahidi kushinda dhuluma za kihistoria na kupata nafasi sahihi ya Afrika duniani. Ruwaza hii inaweza kufikiwa kupitia utatuzi wa migogoro, juhudi za kukabiliana na ugaidi, kukuza biashara ya ndani ya Afrika, kukusanya rasimlimali, kuboresha taasisi, na kutumia uwezo wa Afrika kwa maendeleo endelevu na ya kisasa.

Misri na Kenya zina-shirikiana kikamilifu ili kutatua mizozo na kurejesha amani barani Afrika. Ushirikiano wao wa kiuchumi ni mfano wa kuigwa kwa ushirikiano wa Afrika, ambapo biashara kati ya nchi hizo mbili ilifikia dola milioni

600 mwaka wa 2023 na ongezeko la asilimia tisa katika nusu ya kwanza ya 2024. Misri ni nchi ya pili kwa kuingiza bidhaa nchini Kenya na mshirika wake wa kumi kwa ukubwa wa kibiashara. Nchi hizo mbili zinalenga kupanua ushirikiano wake katika maeneo kama vile teknolojia ya habari na mawasiliano, usimamizi wa maji, uboreshaji wa ardhi, viwanda, dawa, huduma za afya, nishati mbadala, miundomsingi, maendeleo ya miji na masuala ya bahari. Ziara ya kitaifa ya Rais Ruto imeweka msingi wa mikataba mingi baina ya nchi hizo mbili inayolenga kupanua ushirikiano wake na kuvutia uwekezaji zaidi.

Misri na Kenya pia zinafanya kazi pamoja kutekeleza “Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika: Afrika Tunayoitaka” na kurekebisha mfumo wa fedha wa kimataifa. Juhudi zao zinaungwa mkono na uanachama wao katika Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) na mipango ya kieneo kama vile TFTA na AfCFTA.

Mabadilishano ya kitamaduni na kielimu yameimarisha uhusiano

kati ya Misri na Kenya, huku Al-Azhar ya Misri ikitoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Kenya. Utalii pia hutumika kama daraja, huku wageni wa Kenya wakivutiwa na maeneo muhimu ya Misri na watalii wa Misri wakivutiwa na mandhari ya Kenya. Vyuo vikuu 98 vya Misri na vyuo vya kijamii vinawapa vijana wa Kenya fursa za kusomea digrii, huku Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Misri likitoa kozi za mafunzo ya kitaaluma.

Huku Wakenya karibu 3,000 wakiishi Misri, Mkakati wa Soko la Kazi Duniani wa Kenya unalenga kuanzisha makubaliano ya kazi baina ya nchi hizo mbili ili kuwezesha Wakenya wote wanaoishi Misri, wakiwemo wake wa mabalozi, kufanya kazi. Uhusiano wa Misri na Kenya, uliokitwa katika historia ya pamoja na ushirikiano wa kimkakati, unatoa uwezekano wa manufaa ya pande zote kwa mataifa ya Afrika.

*Dkt. Mudavadi ni Mkuu wa Mawaziri na Waziri wa Mashauri ya Kigeni na Diapora Kenya Ilhali Dkt. Abdelatty ni Waziri wa Mashauri ya Kigeni na Uhamiaji wa Misri.*

## Wakulima wa Makueni kuwa wa kwanza kunufaika kupitia mpango wa kupima udongo

NA FAITH NZEMBI, KNA

Wakulima katika Kaunti ya Makueni watanufaika kutokana na mpango wa kitaifa wa kupima sampuli za udongo kidijitali unaoenga kuboresha mapato ya kilimo katika eneo hilo.

Shughuli hiyo, iliyongozwa na Serikali ya Kaunti ya Makueni, Mradi wa Kitaifa wa Kuendeleza Mfumo wa Thamani ya Kilimo (NAVCDP), na Shirika la Utafiti wa Kilimo na Mifugo Kenya (KARLO), unalenga kutathmini ubora wa udongo na kuwapa wakulima taarifa muhimu kuhusu usimamizi wa rutuba ya udongo wao.

Gavana wa Makueni Mutula Kilonzo Jr., ambaye alizungumza wakati

wa uzinduzi huo katika soko la Kwa Kathoka, alisisitiza umuhimu wa mpango huo, akibainisha kuwa afya ya udongo huathiri moja kwa moja mavuno ya mazao na usalama wa chakula. Hii inaashiria hatua kuu katika kushughulikia changamoto za rutuba ya udongo katika wadi zote 30 za kaunti hiyo. Aliwataka wakulima washirikiane

**Shughuli hii ni sehemu ya mpango wa kitaifa wa kugua udongo kidijitali na inalenga kujenga mfumo wa habari kuhusu udongo**

na maafisa wa KARLO wanaoendesha shughuli hiyo huku akiwahakikishia kuwa matokeo yatakayopatikana yatawaelekeza katika matumizi sahihi ya mbolea na mbinu bora za kilimo.

“Ukaguzi wa udongo utasaidia kuamua viwango vya virutubisho na kuwaelekeza wakulima kuhusu uwekaji mbolea ipasavyo,” akasema Gavana Mutula. Mkurugenzi wa KARLO wa Usimamizi wa Mazingira na Maliyasi, Dkt. David Kamau, alisema kupungua kwa rutuba ya udongo kumesababisha wasiwasi mkubwa nchini Kenya, na kufanya afua kama hizo kuwa muhimu kwa kilimo endelevu.

“Zoezi hili ni sehemu ya mpango wa kitaifa wa



Gavana wa Makueni Mutula Kilonzo Jr. wakati wa kuzinduliwa kwa shughuli ya kukagua udongo kidijitali inayolenda kudumisha rutuba ya udongo katika eneo la Kwa Kathoka, Kaunti ya Makueni.

kupima udongo kidijitali ambao unatazamiwa kuunda mfumo wa taarifa za udongo ambao utawaongoza wakulima kuhusu usimamizi wa rutuba ya

udongo,” akasema Dkt Kamau. Shughuli hiyo ya miezi mitatu itashirikiwa vijana 120 wa kilimo—wanne kutoka kila kata—ambao watakuwa

na jukumu la kukusanya sampuli za udongo, kuongeza ufahamu, na kuwaelimisha wakulima kuhusu umuhimu wa kupima udongo.

# Mradi wa maji wa Sh1.2 bilioni wa Makutano – Kenol uliokamilishwa hivi majuzi kufaidi wakazi 70,000

NA FLORENCE KINYUA, KNA

Mradi mpya wa kusambaza maji na maji taka wa Makutano-Kenol utan-ufaisha wakazi zaidi ya 70,000 wa miji ya Makutano, Wempa, Mareira, Karimamwaro, Gatanga, Kabati, Kenol na Wangu.

Mradi huo wa Sh1.2-bilioni ulizinduliwa mwaka wa 2021 chini ya utekelezaji wa Shirika la Ustawi wa Maji Athi (AW-WDA) na ulifadhiliwa na Serikali ya Kenya kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo Afrika (ADB).

Upeo wa mradi huo ulijumuisha utengenezaji wa njia za maji taka zenye urefu wa kilomita 32, njia za maji safi zenye urefu wa kilomita 195, na ujenzi wa matangi ya kuhifadhi maji.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua mradi huo, Afisa Mkuu Mtendaji wa AWWDA Mhandisi Joseph Kamau alisema kuwa mradi huo umekamilika na unatazamiwa kuanza kufanya kazi chini



Afisa Mkuu Mtendaji wa AWWDA, Mhandisi Joseph Kamau, wakati wa ziara ya ukaguzi.

ya Mpango wa Usambazaji Endelevu wa Maji wa Miji Kenya ili kufikia viwango vinavyofaa vya usafi wa mazingira kwa wakazi.

“Kiwanda cha maji taka pia kimekamilika, tuko katika hatua ya mwisho ya ukaguzi, na baada ya hapo kitakabidhiwa kwa kampuni ya maji (MUSWASCO) kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi.

“Kiwanda cha kutibu maji taka kina uwezo wa kutibu mita za ujazo 3,000 za maji chafu kwa siku na kunufaisha familia

zaidi 1000 zinazotarajiwa kuunganishwa kwenye bomba la maji taka, hivyo kuchangia katika mazingira safi,” akasema.

Mhandisi Kamau aliongeza kwamba miunganisho hiyo inatarajiwa kuanza mara moja na itakamilika baada ya miezi miwili.

Vipengele vya miradi hiyo ni pamoja na uwekaji wa bomba la maji taka lenye urefu wa kilomita 17 na bomba la kilomita 15.5 la mitaro ya maji taka.

Mtambo huo wa kud-

hibiti maji machafu unakuja kama afueni kwa wakazi wa miji ya Kenol na Kabati kwani njia hiyo ya maji taka itaunganishwa kwa familia zaidi ya 1,000 kutoka mijini ambayo kwa sasa inategemea matangi ya maji taka ya chini ya ardhi,” akasema.

Kulingana naye, mtambo huo wa kudhibiti maji machafu ni muhimu kwani utatoa mfumo mzuri na wa usafi wa usimamizi na usafi wa mazingira kwa maeneo ya miji ya Kenol-Makutano.

“Tumefanya kazi nyingi katika eneo la juu la mto ili kuhakikisha kuwa usambazaji wa maji kuelekea mjini unapungua chini ya mradi huo na sasa tunakamilisha mtambo wa kusafisha maji machafu ambao utahudumia wakazi katika maeneobunge ya Kandara na Maragua kwani uunganisho wa maili ya mwisho tayari umefanywa Kenol ili kuhudumia watu,” akasema.

Eng. Mhandisi Dickson Nyongesa akielezea



Mradi wa kusambaza maji na kuondoa maji chafu wa Kenol- Makutano.

KNA jinsi matibabu hayo yatakavyofanyika, alisema baada ya taka kupokelewa, itafanyiwa usagaji bila oksijeni kabla ya kwenda hatua ya pili ambapo usagaji wa wa kutumia oksijeni utafanyika hadi hatua ya mwisho.

Aliwatahadharisha wakazi dhidi ya kutumia maji hayo mara moja kutokana na kuwepo kwa bakteria wa kwa kuwa mtambo

huo hauna hatua ambayo maji yanatakiwa kutibiwa kwa dawa.

“Hata hivyo, baada ya maji yaliyosafishwa kuchanganyika na maji mtoni kwa muda, yanakuwa salama kwa matumizi,” akasema.

Uchafu kutokana na mchakato huo unaweza kutumiwa na wakulima katika mashamba yao kama mbolea.



## Actuarial Science Scholarships for Academic Year 2025/2026

The Insurance Regulatory Authority (IRA) is a State Corporation established under the Insurance Act, Cap 487 of the Laws of Kenya with the mandate to regulate, supervise and promote the development of the insurance industry in Kenya.

The Authority is offering eight (8) scholarship opportunities to Kenyan citizens interested in pursuing Master of Science Degree in Actuarial Management at the BAYES Business School, United Kingdom. The scholarship will cater for tuition, travel, accommodation and any other incidental expenses.

### Scholarship for Master of Science Degree in Actuarial Management

Eligible candidates must meet the following requirements:-

1. Should have obtained a Bachelor of Science in Actuarial Science (at least Upper Second-Class Honors) or an equivalent Actuarial Science qualification;
2. Should have graduated not more than Six (6) years ago; and
3. Should have made significant progress towards becoming Associate Members of the Institute /Faculty of Actuaries (Minimum 5 professional papers).

The application forms are available and can be downloaded from the IRA website i.e. [www.ira.go.ke](http://www.ira.go.ke). Completed application forms together with copies of identification, result slips/transcripts, academic certificates, birth certificate and school leaving certificate should be sent to:

The Chief Executive Officer  
Insurance Regulatory Authority  
P.O. Box 43505 GPO 00100, Nairobi, Kenya  
Email: [commins@ira.go.ke](mailto:commins@ira.go.ke)

The applications should reach IRA offices not later than **Friday 28th February 2025, 5.00pm**. Applicants with First Class Honors will have an added advantage.

Note: Only shortlisted candidates will be contacted and canvassing will result in automatic disqualification.



REPUBLIC OF KENYA



## National Environment Management Authority

### NOTIFICATION UNDER SECTION 8 OF THE STATUTORY INSTRUMENTS ACT CAP 2A

### THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT AND CO-ORDINATION (CONSERVATION AND MANAGEMENT OF WETLANDS) DRAFT REGULATIONS, 2025 REGULATORY IMPACT STATEMENT

IT IS HEREBY NOTIFIED TO THE GENERAL PUBLIC of the intention of the Cabinet Secretary Ministry of Environment, Climate change and Forestry to publish the above mentioned Regulations.

The OBJECTIVES of the proposed Regulations include-

- a) To revise the Environmental Management and Coordination (Conservation and Management of Wetlands) Regulations, 2009 and thus provide for conservation of wetlands and their resources in Kenya;
- b) To promote the integration of wise-use of resources in wetlands into local, county, and national planning for, ecological, aesthetic, cultural and socio-economic development;
- c) To ensure the protection of the diversity of wetland habitats, flora and fauna;
- d) To promote awareness creation, education, research, indigenous knowledge and partnerships with other relevant institutions in the management of wetland ecosystems;
- e) To protect wetlands within river basins, lake basins and coastal zones from pollution including siltation, agricultural and infrastructural developments, over exploitation, alien and invasive species, and other activities likely to degrade the wetland ecosystem.

A draft of the proposed Regulations and the Regulatory Impact Statement may be accessed from [www.nema.go.ke](http://www.nema.go.ke). Link: <https://shorturl.at/2U76>

Comments on the proposed Regulations are hereby invited from the general public through written memoranda addressed to [emcareview@gmail.com](mailto:emcareview@gmail.com) or [legalnema@gmail.com](mailto:legalnema@gmail.com) and to be submitted by close of day on the **25th February, 2025**.

Public participation meetings will thereafter be held physically in regional venues that will soon be notified to the public.

Mamo B. Mamo, EBS  
Director General



: @ NemaKenya





REPUBLIC OF KENYA

### JOB VACANCIES (REPLACEMENT)

The Nuclear Power and Energy Agency is seeking to recruit open-minded, self-driven and results-oriented individuals of high integrity to fill the following positions:

| S/No. | Reference No.          | Position                                          | Grade   | Posts | Terms of Employment                                                        |
|-------|------------------------|---------------------------------------------------|---------|-------|----------------------------------------------------------------------------|
| 1.    | NuPEA/DIAC/01/01/ 2025 | Director, Information, Advocacy and Communication | NuPEA 2 | 1     | Five (5) years contract renewable once subject to satisfactory performance |
| 2.    | NuPEA/MS/01/01/ 2025   | Manager, Supply Chain                             | NuPEA 3 | 1     | Three (3) years contract renewable subject to satisfactory performance.    |
| 3.    | NuPEA/SLO/01/01/ 2025  | Senior Legal Officer                              | NuPEA 5 | 2     | Permanent and pensionable terms of service.                                |
| 4.    | NuPEA/IA/01/01/ 2025   | Internal Auditor                                  | NuPEA 6 | 1     | Permanent and pensionable terms of service.                                |
| 5.    | NuPEA/AOA/01/01/ 2025  | Assistant Office Administrator                    | NuPEA 7 | 1     | Permanent and pensionable terms of service.                                |

For more information on the application procedure, kindly visit the Agency's website; [www.nuclear.co.ke](http://www.nuclear.co.ke). Applications to be sent through post or delivered to the following address: -

**The Chief Executive Officer**  
**Nuclear Power and Energy Agency**  
**Kawi Complex, 4th Floor**  
**Popo Road, South C, along Red Cross Road**  
**P.O. Box 26374-00100 NAIROBI**

or

**emailed to [recruitment@nuclear.co.ke](mailto:recruitment@nuclear.co.ke).**

Applications must be received by **5.00 pm** on **4th March, 2025**. Canvassing in any manner shall lead to automatic disqualification. Only shortlisted candidates will be contacted.

**NuPEA is an Equal Opportunity Employer committed to diversity and gender equality.**



REPUBLIC OF KENYA

### KENYA INSTITUTE OF CURRICULUM DEVELOPMENT

*Nurturing Every Learner's Potential*

### VACANCIES

The Kenya Institute of Curriculum Development wishes to recruit qualified professionals for various vacant positions as outlined below.

| S/NO | POSITION                                                                 | KICD GRADE | NO. OF POSTS |
|------|--------------------------------------------------------------------------|------------|--------------|
| 1    | Chief Principal Curriculum Development Officer, Primary Education        | 3          | 1            |
| 2    | Chief Principal Curriculum Development Officer, Secondary Education      | 3          | 1            |
| 3    | Deputy Director, Internal Audit                                          | 3          | 1            |
| 4    | Senior Principal Curriculum Development Officer                          | 4          | 4            |
| 5    | Assistant Director, Supply Chain Management                              | 4          | 1            |
| 6    | Assistant Director, Legal Services                                       | 4          | 1            |
| 7    | Principal ICT Officer                                                    | 5          | 1            |
| 8    | Curriculum Development Officer, CRE Primary Education                    | 6          | 1            |
| 9    | Curriculum Development Officer, Mathematics-Secondary Education          | 6          | 1            |
| 10   | Curriculum Development Officer, French- Secondary Education              | 6          | 1            |
| 11   | Curriculum Development Officer, Physical Education – Secondary Education | 6          | 1            |
| 12   | Curriculum Development Officer, Theatre and film- Secondary Education    | 6          | 1            |
| 13   | Curriculum Development Officer, Hindu Religious Education                | 6          | 1            |
| 14   | Senior Security Officer                                                  | 6          | 1            |
| 15   | Principal Studio Technical Operator                                      | 6          | 1            |

Interested applicants should forward their application letters, copies of academic and professional certificates, testimonials, up-to-date curriculum vitae and ID card to the address below to be received not later than **3<sup>rd</sup> March, 2025**.

All applicants should give full details of their addresses including mobile telephone numbers as well as names and addresses of two referees. More details can be obtained from KICD Website: [www.kicd.ac.ke](http://www.kicd.ac.ke).

**The Director/Chief Executive Officer,**  
**Kenya Institute of Curriculum Development,**  
**P.O. Box 30231-00100**  
**NAIROBI**

NB: Only shortlisted candidates will be contacted and any canvassing will lead to automatic disqualification.

**We encourage people with disability and the marginalized to apply.**



REPUBLIC OF KENYA

### DECLARATION OF VACANCIES

Pursuant to the provisions of section 17 (1) of the NPSC Act, 2011 (revised 2014) and Article 10 and 232 of the Constitution of Kenya, the Commission seeks to competitively fill vacant positions in the establishment.

Subsequently, the Commission invites applications from qualified persons to fill the following positions at the National Police Service Commission Headquarters and Regional Offices:-

| S/No | Vacancy                                               | Reference     | No. of Posts |
|------|-------------------------------------------------------|---------------|--------------|
| 1.   | Director, Information, Communication Technology (ICT) | V/No. 1/2025  | 1            |
| 2.   | Director, Finance & Administration                    | V/No. 2/2025  | 1            |
| 3.   | Deputy Director, Finance & Accounts                   | V/No. 3/2025  | 1            |
| 4.   | Manager, Internal Audit                               | V/No. 4/2025  | 1            |
| 5.   | Manager, Administration                               | V/No. 5/2025  | 1            |
| 6.   | Manager, Supply Chain Management                      | V/No. 6/2025  | 1            |
| 7.   | Senior Counselor                                      | V/No. 7/2025  | 20           |
| 8.   | Counselor II                                          | V/No.8/2025   | 20           |
| 9.   | Human Capital Management Officer II                   | V/No. 9/2025  | 10           |
| 10.  | Human Capital Management Assistant                    | V/No. 10/2025 | 8            |
| 11.  | Record Management Officer II                          | V/No. 11/2025 | 8            |
| 12.  | Record Management Officer III                         | V/No. 12/2025 | 6            |
| 13.  | Social Worker II                                      | V/No. 13/2025 | 10           |
| 14.  | Social Worker III                                     | V/No. 14/2025 | 6            |
| 15.  | Information Officer II                                | V/No. 15/2025 | 6            |
| 16.  | Finance Officer II                                    | V/No. 16/2025 | 3            |
| 17.  | Economist II                                          | V/No. 17/2025 | 3            |
| 18.  | Account Assistants III                                | V/No. 18/2025 | 8            |
| 19.  | ICT Officer II                                        | V/No. 19/2025 | 6            |
| 20.  | ICT Officer III                                       | V/No. 20/2025 | 4            |
| 21.  | Supply Chain Management Officer II                    | V/No.21/2025  | 4            |
| 22.  | Supply Chain Management Assistant                     | V/No.22/2025  | 4            |
| 23.  | Clerical Officer II                                   | V/ No.23/2025 | 10           |
| 24.  | Office Assistants                                     | V/No. 24/2025 | 7            |
|      | <b>Total</b>                                          |               | <b>149</b>   |

**Mode of application**

i. Interested and qualified persons are requested to make their applications **ONLINE** through jobs portal: <https://service.npsc.go.ke/recruitment>

Detailed Job Descriptions to be obtained at the Commission website; [www.npsc.go.ke](http://www.npsc.go.ke)

**Other Requirements**

i. Shortlisted candidates will be expected to bring the original certificates for verification during the interview.

ii. Shortlisted candidates for the position of Managers and above will be required to satisfy the requirement of Chapter Six (6) of the Constitution of Kenya 2010 by obtaining clearance certificates from KRA, HELB, EACC, CRB and DCI.

Applications should be addressed to:

**The Commission Secretary/ Chief Executive Officer**  
**National Police Service Commission**  
**CBK Pension Towers, Harambee Avenue**  
**P.O Box 47363-00100 Nairobi**

So as to reach the Commission by the close of business on or before **21<sup>st</sup> February, 2025 at 5.00 pm East African Time (EAT).**

**NB: National Police Service Commission is an equal opportunity employer committed to diversity and gender equality. Persons with disabilities and from disadvantaged groups are encouraged to apply. Only qualified candidates shall be contacted.**

**Any form of canvassing shall lead to automatic disqualification**

**Peter Leley, EBS**  
**CS/Chief Executive Office**  
**National Police Service Commission**

---

**Vision**  
*A Dignified and Professional Police Officer*

# Faida ya KenGen yapanda kwa asilimia 79 kufuatia hatua za kukata gharama

NA MATHEW CHEPKEWEL (MYGOV)

Kampuni ya Kuzalisha Umeme Kenya (KenGen), mzalishaji mkubwa wa umeme katika eneo la Afrika Mashariki, imeripoti ukuaji wa asilimia 79 ya faida baada ya ushuru kwa muda wa miezi sita iliyomalizika Desemba 31, 2024, ikiangazia uthabiti wa kampuni hiyo katika mabadiliko ya mazingira ya nishati.

Mzalishaji huyo wa kawi alichapisha faida halisi ya Sh5.30 bilioni, kutoka Sh2.96 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka jana - faida iliyochochewa hasa na hatua kali za kupunguza gharama na kuboreshwa kwa utendakazi.

Wakati huo huo, KenGen ilipata ongezeko la asilimia 49.4 la faida ya uendeshaji, na kufikia Sh6.65 bilioni, kutoka Sh4.45 bilioni katika kipindi cha awali.

Uboreshaji huu ulichochochewa na punguzo la



Mhandisi Peter Njenga, Afisa Mkuu Mtendaji wa KenGen

asilimia 13.7 la gharama za uendeshaji, ambazo zilishuka hadi Sh17.67 bilioni kutoka Sh20.47 bilioni. Mapato, kwa upande mwingine, yalibakia kuwa Sh27.5 bilioni. "Utendaji huu ni uthibitisho wa nidhamu ya kifedha ya KenGen na kuzinga-

tia ufanisi kimkakati," akasema Mhandisi Peter Njenga, Afisa Mkuu Mtendaji wa kampuni hiyo. "Tunaboresha mali zetu, kurahisisha shughuli, na kutumia uongozi wetu katika nishati mbadala ili kuhakiisha thamani ya muda mrefu kwa wenyehisa wetu na nchi," akaongeza.

Mapato ya kifedha ya kampuni hiyo yalipanda hadi Sh2.45 bilioni kutoka Sh1.87 bilioni, yaki-

## 2.9B

**Faida Halisi ambayo kampuni ya kutengeneza umeme ya KenGen ilipata mwaka uliopita**



chochewa na faida kubwa kutokana na uwekezaji wa pesa taslimu na shilingi ya Kenya ambayo iliimarika zaidi. Wakati huo huo, gharama za kifedha zilishuka hadi Sh1.13 bilioni kutoka Sh1.49 bilioni, kuonyesha usimamizi bora wa mtaji na uboreshaji wa deni.

KenGen inabakia kuwa mstari wa mbele katika mpito wa nishati mbadala nchini Kenya, ikisambaza 4,291 GWh za umeme katika kipindi cha nusu

mwaka, kutoka 4,211GWh katika kipindi kilichopita.

Alisema kuwa KenGen inalenga kupanua mfumo wake wa nishati mbadala chini ya mkakati wake wa G2G 2034, mwongozo wa muda mrefu unaoenga kuimarisha mpito wa nishati ya kijani nchini Kenya.

Kati ya 2025 na 2027, kampuni hiyo inapanga kuongeza 194.4MW ya uwezo uliowekwa kwenye miradi ya mvuke, maji na nishati ya jua, pamoja

na 100MWh ya uhifadhi wa nishati ya betri ili kuimarisha uthabiti wa mfumo wa kitaifa, akadokeza.

Mapato ya KenGen kwa kila hisa (EPS) yalipanda kwa asilimia 78 hadi Sh0.80, kutoka Sh0.45, na hivyo kuimarisha uwezo wa kampuni hiyo kuunda thamani ya wanahisa katika soko linalobadilika la nishati. "Tunaendesha mustakabali wa nishati nchini Kenya," akasema Njenga.



**NEW KENYA CO-OPERATIVE CREAMERIES LTD**

Creamery House  
Dakar Road Industrial Area  
P.O Box 30131-00100, Nairobi Kenya  
Tel: 020 3980000  
Email: info@newkcc.co.ke  
Website: www.newkcc.co.ke

## TENDER NOTICE

Tenders are invited from interested and eligible firms/suppliers to submit sealed bids for following:

| No | Tender Number          | Description                                                                                | Eligibility | Closing/Opening Date |
|----|------------------------|--------------------------------------------------------------------------------------------|-------------|----------------------|
| 1  | NKCC.FAW.038.2024/2025 | Provision of Transport Services for Finished Products (Sales & Distribution)               | Open        | 26th February 2025.  |
| 2  | NKCC.FAW.039.2024/2025 | Provision of Transport Services - Packaging Materials & Detergents.                        | Open        | 26th February 2025.  |
| 3  | NKCC.FAW.040.2024/2025 | Provision of Transport Services- Finished Products (Intercreamery-Long Life and Fermented. | Open        | 26th February 2025.  |
| 4  | NKCC.FAW.041.2024/2025 | Provision of Transport Services - Raw milk Haulage (Truck and Tanker)                      | Open        | 26th February 2025.  |
| 5  | NKCC.FAW.042.2024/2025 | Provision of Transport Services - Raw milk Haulage (Prime Mover only)                      | Open        | 26th February 2025.  |
| 6  | NKCC.FAW.043.2024/2025 | Provision of Transport Services - Bulk Water.                                              | Open        | 26th February 2025.  |
| 7  | NKCC.FAW.044.2024/2025 | Provision of Transport Services - Furnace Oil.                                             | Open        | 26th February 2025.  |

Complete Tender document with detailed information may be obtained from the **Office of Head of Procurement, New KCC Ltd, Creamery House, Dakar Road off Enterprise Road between 9.00 a.m. to 4.00 p.m., upon payment of a non-refundable fee of Kshs. 1,000/- (Kshs. One Thousand only) per tender document**, paid in cash or Bankers Cheque. Prospective bidders may also download the Tender documents from PPIP portal <https://tenders.go.ke> or New KCC Website [www.newkcc.co.ke](http://www.newkcc.co.ke) free of charge. Interested bidders are required to register by e-mailing their company name and contact details to: [procurement@newkcc.co.ke](mailto:procurement@newkcc.co.ke) and [info@newkcc.co.ke](mailto:info@newkcc.co.ke)

Completed Tender documents in plain sealed envelope clearly marked with Tender Number and Description should be addressed to:

**Ag. Managing Director  
New KCC Ltd  
P.O. Box 30131-00100 Nairobi.**

To be received no later than **10.00 a.m** on the **26<sup>th</sup> February 2025** and to be opened immediately in the presence of any bidder's representative who chooses to attend.



**COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA**

## PUBLIC NOTICE

### PUBLICATION OF THE NATIONAL TABLE OF FREQUENCY ALLOCATIONS

The Communications Authority of Kenya (CA) is the regulatory agency for the ICT industry in Kenya with responsibilities in telecommunications, cyber security, e-commerce, broadcasting and postal/courier services. CA is also responsible for managing the country's numbering and frequency spectrum resources, administering the Universal Service Fund (USF) as well as safeguarding the interests of users of ICT services.

The Authority under the Kenya Information and communications Act, 1998 and its attendant Regulations, is responsible for the management of Kenya's radio frequency resource to facilitate the deployment of efficient radio-communication technologies and services.

In the execution of the said mandate, the Authority regularly reviews existing spectrum uses as well as strategic planning for the future use of the radio spectrum to support the realization of the country's socio-economic development.

The Authority reviews the frequency uses every four years following outcomes of the International Telecommunication Union (ITU) World Radiocommunication Conferences (WRCs).

The WRCs review and, if necessary, revise the Radio Regulations. The Radio Regulations provide an agreed framework of rights, obligations and procedures applicable between countries in their many uses of the radio frequency spectrum. The Regulations also contain the international Table of Frequency Allocations indicating the allocation of radio frequencies to specific radiocommunication services across the world.

The Authority is therefore pleased to present the 2024 edition of the National Table of Frequency Allocations (TOFA) which details the use of various frequency bands pursuant to the World Radiocommunications Conference, 2023 (WRC-23).

The TOFA provides a guide to all spectrum users providing radiocommunications services in the country.

Stakeholders can access the Table of Frequency Allocations on the Authority's website at this link: <https://www.ca.go.ke/licensing-procedures>.

**David Mugonyi, EBS  
DIRECTOR GENERAL & CEO**

Head Office  
CA Centre  
P.O. Box 14448  
Nairobi 00800  
Mobile: 0703042000  
Email: info@ca.go.ke

Western Regional Office  
1<sup>st</sup> Floor KVDA Plaza  
P.O. Box 2346  
Eldoret 30100  
Mobile: 0703042105  
Email: wro@ca.go.ke

Coast Regional Office  
3<sup>rd</sup> Floor, NSSF Building  
P.O.Box 8041  
Mombasa 80100  
Mobile: 0703042152  
Email: cro@ca.go.ke

Central Regional Office  
Ground Floor, Advocates Plaza  
P.O Box 134 Nyeri 10100  
Mobile: 0703042181  
Email: cero@ca.go.ke

Nyanza Regional Office  
2<sup>nd</sup> Floor Lake Basin Mall,  
P.O Box 2016  
Kisumu 40100  
Mobile: 0703042130  
Email: nro@ca.go.ke



@newkcckenya

New Kenya Co-operative Creameries

Life's goodness everyday!

# Hospitali ya Level 4 ya Sh700 milioni kujengwa katika Kaunti Ndogo ya Kuria Mashariki

NA MAKOKHA KHAOYA, KNA

Kaunti ya Migori hivi karibuni itakuwa na hospitali ya pili ya kiwango cha Level 4 kufuatia hafla ya kuweka jiwe la msingi wa hospitali mpya ya orofa tano ya Kegonga katika Kaunti Ndogo ya Kuria Mashariki. Gavana wa Migori Ochilo Ayacko, aliyenongoza hafla hiyo katika Hospitali ya Kaunti Ndogo ya Kegonga, alikiri kuwa hospitali hiyo ya vitanda 300 itakuwa hatua muhimu katika kuendeleza miundomsingi ya afya na kutoa huduma bora za matibabu kwa wakazi. Mradi huo unaofadhiliwa na Wizara ya Afya, utawakilisha maendeleo makubwa katika kuboresha huduma za afya Migori. Gavana Ayacko alipongeza juhudi za Mbunge wa Kuria Mashariki, Kitayama Maisori, kwa ushawishi wake bila kuchoka kuhakikisha kuwa eneobunge lake linapokea miradi ya kimaendeleo. Gavana pia alieleza kuwa ataendelea kus-



Gavana wa Migori Ochilo Ayacko akiweka jiwe la msingi la hospitali mpya ya Level 4 katika Kaunti Ndogo ya Kegonga.

hirikiana na serikali ya kitaifa ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa kuwekeza katika vituo vya kisasa na kupanua upatikanaji wa huduma bora za matibabu. “Mradi huu utakapokamilika utaimarisha utoaji wa huduma kwa kiasi kikubwa, kupunguza msongamano wa wagonjwa, na kuboresha matokeo ya huduma za afya katika eneo hili,” akasema Ochilo. Alisema serikali yake imejitolea kutoa huduma za kipekee za afya kwa kuajiri wafanyakazi waliokitimu.

Mnamo Desemba 2024, kaunti hiyo iliajiri wataalamu 80 wa kusaidia kuboresha huduma katika vituo 167 vya afya katika kaunti hiyo. “Tunaposonga mbele, tutahakikisha hospitali hiyo ina vifaa kamili na wafanyakazi ili kutoa huduma bora kwa wakazi wa kaunti yetu,” akasema Ochilo. Mbunge wa Kuria Mashariki Kitayama Maisori alisema ni kupitia utawala bora na ushirikiano na ngazi zote mbili za serikali ambapo ajenda ya kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi inaweza kutekelezwa.



## POSTGRADUATE COURSES: MAY 2025 INTAKE

